**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Januari, 2026**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**


Anwani ya simu "**MKUU WA SHULE**"
Simu nambari: **0717248404**
Barua pepe: lindigirls@gmail.com

SHULE YA SEK- LINDI WASICHANA
S.L.P. 50
**LINDI**


JINA LA MWANAFUNZI: ……………………………

S.L.P…………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI LINDI WASICHANA MWAKA 2026**

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2026. Shule hii ni ya Bweni maalum kwa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wasichana. Shule ina mandhari na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Shule ya Sekondari Lindi Wasichana (Lindi Girls) iko umbali wa mita **800** kutoka barabara kuu ya Lindi - Dar es salaam katika Kijiji cha Kilangala B. Aidha, Shule ipo umbali wa kilometa takribani **40** toka Lindi Mjini. Ili uweze kufika shuleni kwa urahisi kutokea Dar es salaam, panda mabasi yaendayo Lindi/ Mtwara/ Masasi/ Tunduru/ Nachingwea/ Ruangwa shuka kijiji cha Kilangala (kabla hujafika Lindi mjini). Kutoka stendi ya kijiji cha Kilangala B hadi shuleni kuna umbali wa **mita 800.** Tumia usafiri bodaboda hadi kufika shuleni kwa Tshs **1,000/=**

Muhula wa masomo utaanza tarehe **05 Januari 2026**, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **04 Januari 2026** kabla au ifikapo saa **10:00 alasiri.**
Endapo utabadilisha shule/kwenda shule binafsi, tafadhali tujulishe ili tuweze kuhamisha taarifa zako kwenye mfumo wa Usajili (PREMS) na kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili kujaza nafasi iliyowazi.

***KARIBU SANA*.**

## 1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1.1 SARE YA SHULE

(a) Mwanafunzi aje na sare zenye muonekano ufuatao:

- Sketi 2 za rangi ya **Dark Green** zenye **linda la box mbele na nyuma na malinda pembeni** kwa mbele ziwe ndefu hadi chini. Kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sentimeta 18 au nchi 7 na nusu;
- Sketi zake zisiwe na mkanda (belt) mpana, upana wa belt usizidi sentimenta 5 au nchi moja na nusu. Sketi isibane iwe na upana wa kutosha kumwezesha mwanafunzi kuwa huru.
- Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa;
- Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi tetroni, kwa waislamu blauzi nyeupe mbili (2) mikono mirefu

(b) Viatu vyeusi (visiwe na kisigino kirefu-high heels) jozi mbili (2);

(c) Soksi nyeupe jozi mbili wakati wa masomo na soksi nyeusi jozi mbili kwa ajili ya michezo na wakati wa usiku (Preparation)

(d) Kwa wanafunzi wa kiislamu: blauzi nyeupe ndefu na yenye mikono mirefu. Hijabu ya tetroni nyeupe/juba na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.

(e) Bukta nyeusi kwa ajili ya michezo

(f) Raba nyeusi kwa ajili ya michezo

(g) Truck suit dark blue isiyobana kwa ajili ya maandalizi ya jioni

(h) T-shirt moja (1) ya rangi ya dark blue

(i) Shamba dress mbili (2) rangi ya damu ya mzee/Maroon. Liwe gauni lililoshuka chini lisilobana, liwe zito sio jepesi.

(j) Sweta moja rangi ya dark blue

(k) T-shirt za shule zenye nembo ya shule zitapatikana shuleni kwa sh 15000/= tu, iletwe mkononi.

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:**

i. Awe na sanduku (nunua sanduku la bati) linalofunga vizuri;
ii. Aje na godoro moja la futi 3 kwa 6
iii. Blanketi moja la futi 3 kwa 6
iv. Shuka mbili za kulalia za futi 3 kwa 6 (Pink na Blue Bahari);
v. Foronya ya pink/blue bahari isiyo na maua au urembo wowote;
vi. Awe na chandarua/net futi 3 kwa 6 rangi nyeupe
vii. Taulo za kike za kutosha
viii. Taulo la kuogea/bafuni rangi yoyote
ix. Koti la mvua au mwamvuli
x. Kandambili kwa ajili ya kuogea
xi. Viatu vya plastiki (yebo) rangi yoyote vya kushindia
xii. Gumboots (rain boots/viatu vya mvua)
xiii. Aje na jembe moja na mpini wake
xiv. Aje na soft broom moja
xv. Aje na Hard broom moja
xvi. Aje na Mfagio wa kukaushia maji (drier) moja
xvii. Fagio la chelewa moja la mti
xviii. Fyekeo moja
xix. Brush ngumu moja ya kusugulia choo yenye mpini wa mbao/mti kwa ajili ya kusafishia sinki la choo
xx. Sabuni ya maji kusafisha chooni lita mbili.
xxi. Sabuni ya kuondoa madoa ya uchafu chooni ARO moja.
xxii. Aje na Ndoo ndogo mbili (kwa matumizi ya shule na matumizi binafsi)
xxiii. Awe na container lenye mfuniko/sahani, bakuli, kikombe na kijiko
xxiv. Daftari (kaunta books) Quire three zisizopungua kumi na moja (11)
xxv. Ream moja ya karatasi A4 (photocopy paper) kila muhula.

xxvi. Mathematical set moja kwa matumizi yake awapo darasani;

xxvii. Graph pad moja kwa mwaka

xxviii. Aje na kamusi (dictionary) ya lugha ya kiingereza (English to English)

***TAARIFA: Kwa mahitaji ya vifaa vya kujifunzia (Ream, daftari counter books, dictationary,pen n.k), stationary ipo karibu na shule pia vifaa vya usafi na malazi (shuka, godoro n.k) vinapatikana katika maduka karibu na shule.***

xxix. Picha passport size 4 alizovaa shati ya shule zilizopigwa hivi karibuni zikiwa na "Background" ya Light Blue

xxx. Kama ana bima ya afya aje nayo na kama hana, mzazi au mlezi mkatie

kabla ya kuripoti. Aidha, shule inao utaratibu wa kuwakatia Bima ya afya ya NHIF wakiwa shuleni kwa gharama ya **Tsh. 50,400/=** tu, malipo ya bima yafanyike kupitia **AKAUNTI NAMBA 0150774259600** (**LINDI GIRLS SECONDARY SCHOOL**), benki ya **CRDB** na mwanafunzi afike na risiti/hati ya kuweka fedha benki. **Hatutapokea mkononi**.

## 2.0 CHAKULA

Kama zilivyo shule zote za bweni za serikali, shule ya sekondari Lindi Wasichana hutoa chakula safi na salama ambacho serikali imeelekeza kitolewe. Endapo unayo miiko ya kutokula baadhi ya vyakula, shule haitatoa huduma ya chakula Maalum (pekee) kwa kila mwanafunzi. Aidha, Pia shule haitoi kibali cha mwanafunzi kujipikia na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/kinywaji kutoka nje.

## 3.0 NGUO NYINGINE

- Mwanafunzi aje na khanga au kitenge doti moja tu, mwanafunzi aje kuripoti akiwa amevaa sare ya shule, shamba dress au track suit (dark blue). Mwanafunzi hatapokelewa endapo atakuja na nguo za nyumbani;
- Endapo mwanafunzi atabainika kuwa na nguo zisizoruhusiwa akiwa shuleni, atarudishwa nyumbani kurejesha nguo hizo kwa gharama zake.
- Aidha. Masanduku/mabegi makubwa hayaruhusiwi, kwani shule haina nafasi ya kuyatunza**. Mwanafunzi akifika nalo atalazimika kulirudisha nyumbani kwa gharama zake.**

## 4.0 MAELEZO YA ZIADA KWA MZAZI/MLEZI

(a) Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia (WyEST), hivyo Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto wako anaripoti kwa wakati shuleni;

(b) Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia simu ya mkuu wa shule;

(c) Maombi ya ruhusa ya mwanafunzi kurejea nyumbani yapitie ofisi ya Mkuu wa shule; Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa sababu za lazima tu mfano Matibabu au Msiba wa Wazazi/Walezi.

(d) Shule haina utaratibu maalum wa kuwatembelea wanafunzi (parenting visisting day) bali kuna mawasiliano kati ya mwanafunzi na mzazi kupitia mwalimu wa darasa kila mwisho wa mwezi mara moja tu (weekend ya mwisho wa mwezi)

(e) Wakati wa Likizo, mwanafunzi wote watalazimika kurejea nyumbani

## 5.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo amabayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kufika shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

(d) Kuwahi kwa kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(i) Kutunza mali za shule

(j) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari/Mtaalamu wa Afya;

(k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

(l) Mwanafunzi hataruhusiwa kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(m) Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika bwalo

(n) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi atakayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi

(o) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu

## 5.1. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga/usagaji
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu;
iv. Kutoa lugha chafu na zisizo na utu/maadili kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Ubakaji
vi. Ulevi;
vii. Matumizi ya vilevi na madawa ya kulevya kama vile pombe, bangi, sigara, n.k
viii. Kupigana na mwanafunzi, mwalimu au mtu yeyote yule;
ix. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba au kusaidia vitendo vya kutoa mimba;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa;
xiv. Kumiliki, kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kukataa/kudharau adhabu iliyotolewa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua;
xvii. Kutokuhudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila sababu za msingi;

## 6.0. VIAMBATANISHO MUHIMU VINAVYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI

- Fomu ya kupimwa afya yake (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Foumu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule
- Picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa wanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**TAHADHARI;**

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya utapeli (wizi kwa njia ya mtandao) yanayohusisha wanafunzi waliopo shule za bweni. Hivyo, unasisitizwa kuwa;

***Upatapo ujumbe/Taarifa yoyote kuhusu Mwanafunzi/Mtoto wako, Tafadhali usitume chochote kwa Mhusika kabla ya kuwasiliana na Uongozi wa shule ili kupata taarifa sahihi.*** **Kwa mawasiliano yote, Tafadhali wasiliana na wafuatao;**

1. **MKUU WA SHULE** 0717248404
2. **MAKAMU MKUU WA SHULE** 0782208844
3. **MWALIMU WA TAALUMA** 0717927797

***"LINDI GIRL..!!! SAYANSI NA WASICHANA KWA MAENDELEO YA TAIFA"***

**……………….**

**JENNIFER VALENTINO SUNGU**

**MKUU WA SHULE- LINDI WASICHANA SEKONDARI**

**FORM NO.1: MEDICAL EXAMINATION**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Lindi Girls Secondary School

P.O BOX 1070

LINDI.

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**.

Please examine Miss …………………………………………………………………… as her physical and Mental fitness for admission as a form …………………….. Students at Lindi Girls' Secondary School in the year ………………

Your sincerely.

HEADMISTRESS

The headmistress,

I have examined Miss ………………………………………………………… as shown and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time secondary school education.

1. Vision with/without glasses. Right ……………………… Left ………………………
2. Blood pressure …………………………… Hemoglobin ………………………
3. Hearing ………………………………………………………
4. Urine (a) Albumen………………………… (b) ............................
5. a) Venereal diseases…………………(b) Bilharzia............................
6. Pregnancy ……………………………………………………………
7. Neurosis……………………………………………………………
8. Is there any abnormality of : (a) The heart……………………………
   b) Lungs ……………………… c) The spleen …………………
9. Are there serious diseases. E.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes, etc. ……………………………………………………………………………..

Date ……………… Signature of the medical Officer ………………

Station …………………                    Designation ……………………

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI.**

1. (a) Jina la mwanafunzi ………………………………………………….. (b) Anuani …………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………..
3. Shule aliyomalizia darasa la saba …………………………
   Mwaka …………………………………………….
4. Mkoa anaotoka ………………………… Wilaya alipozaliwa ……………………………..
5. Tarafa anayotoka ……………………….. Kata atokayo ……………………
6. Kijiji anachotoka ………………………….. Mtaa anaotoka ……………… 7. Jina la Mtendaji wa (a) Kata ………………………. (b) Mtaa/Kijiji ………
8. Jina la (a) Balozi wa nyumba kumi ……………………….
   (b) Mwenyekiti wa Mtaa ……………………………
9. Michezo anayopendelea

| Na. | Jina la Mchezo |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |

11. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| Na. | Aina ya Uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo na sitapata chini ya alama 50 chini ya 100 kwa kila mtihani,zoezi au jaribio nitakalofanya hapa shuleni

**Jina la Mwanafunzi …………………………………….. Sahihi ……………….**

**Tarehe ………….**

## FOMU NAMBA 3.
## TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi …………………………………………………..
2. Kazi anayofanya mzazi ……………………………………………………
3. Anuani ………………………………………………………..
4. Namba ya simu ……………………………………
5. Mkoa ……………………..Wilaya ……………… Tarafa …………………

Kata ……………………………… Kijiji …………………….Mtaa ……………

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mwanafunzi atakuwa anakwenda wakati wa likizo

   Mahali ……………………………………. kwa nani ……………………

7. Majina ya viongozi/Wazazi /walezi atakakokuwa anakwenda wakati wa likizo
   - Jina la Baba /mlezi/ndugu ………………………………………..
   - Jina la mama/mlezi …………………………………………………….
   - Mtendaji wa Kata ………………………………………….….
   - Mtendaji wa Kijiji/Mtaa …………………………………….……
   - Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa ……………………………………………

**TAMKO LA MZAZI**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………… ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Lindi Wasichana katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya. Ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule pale itakapobidi.

**Jina la Mzazi/Mlezi ……………….Sahihi ……...…… Tarehe ……………**

**FOMU NA.4**

**FOMU MAALUM YA TAARIFA ZA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

Ndugu wa karibu wa mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao.

Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea.

**(Ambatanisha passport size 4 za ndugu wa karibu)**

**1. (a)Jina ___________**
(b)Uhusiano: ____________________________
(c) Anwani:______________________________________________
(d)Namba ya Simu:_____________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: ______________________
Tarehe: ____________________________

**2 .(a)Jina**___________________________________________
(b) Uhusiano: ________________________________________
(c) Anwani:_____________________________________________
(d) Namba ya Simu:___________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: ______________________
Tarehe: ____________________________

**3. (a)Jina**________________________________________________ (b)
Uhusiano: _____________________________
(c) Anwani:_____________________________________________
(d) Namba ya Simu:__________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: ______________________
Tarehe: ____________________________

**4. (a)Jina**________________________________________________ (b)
Uhusiano: _____________________________
(c) Anwani:_____________________________________________
(d) Namba ya Simu:__________________________________
Saini ya mzazi/Mlezi: ______________________
Tarehe: ____________________________

## FOMU NAMBA 5
## MKATABA/TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi…………………………………………………………………..……

(jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyoelekezwa katika fomu hii. Nitatii na kufuata sheria zote za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai na makosa mengine yaliyotajwa. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuhakikisha ninapata ufaulu wa Alama za juu hususani katika masomo ya Sayansi na kuendelea na Kidato cha Tano. Aidha, naahidi kuwa na ushirikiano mzuri na wanafunzi wenzangu na kuwa mfano bora wa Taasisi ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Lindi (Lindi Girls) ndani na nje ya shule.

**Saini ya mwanafunzi** ……………………………………………………

**Tarehe**………………………………………